

جمعية الدعوة والإرشاد وتنمية المجالس بالزلفي
مشروع تَعْلُمُ الْإِسْلَام – أحكام الطهارة - سواحيلي

Samo la 1

الدرس الأول

TWAHARA NA NAJISI.

NAJISI YA HISIYA, ni najisi ambayo ni wajibu juu ya muislamu kuisafisha na kuiondoa na kuosha sehemu iliyopatwa na najisi hiyo.

Ni wajibu kusha nguo na mwili viliyoingiwa na najisi hiyo mpaka iondoke sehemu iliyointingia, ikiwa najisi hiyo inaonekana kama vile damu ya hedhi itaoshwa, ikiwa itabakia athari yake kutokana na ugumu wa kutoka basi itachwa hakuna tatizo kwa kubaki kwa athari hiyo.

Ikiwa najisi haionekani inatosha kuosha sehemu hiyo hata kama ni mara moja inatosha.

Ikiwa najisi imesambaa ardhini kutwaharishwa kwake ni kumwaga maji juu yake, kama ambavyo kutwaharishwa kwake ni kukauka kwa najisi ikiwa ni ya umajimaji.

Ama ikiwa najisi ni ya athari sio maji maji haitwaharishwi kwa maji isipokuwa itaondolewa na kwenda kutupwa kama vile kinyesi cha mbwa n.k.

Hutumika maji katika kutwaharisha na kuiondoa najisi, kama vile maji ya mvua, maji ya bahari, maji yam to na maji mengineyo ambayo ni twahara.

Kama ambavyo inafaa kuyatumia maji yaliyotumika ambayo hayaja badilika na vile vile inafaa kuyatumia maji ambayo yamechanganyika na kitu ambacho ni twahara, maji yatabaki katika asili yake hayatabadilika.

Lakini maji yakichanganyika na kitu ambacho ni twahara lakini yakabadilika maji kutoka kwenye asili yake ya maji hayatafaa kujitwaharisha, kama vile soda, chai n.k.

Vile vile haifai kuyatumia maji yaliyo changanyika na najisi, ikawa najisi imeyabadilisha maji ladha yake, harufu yake na rangi yake.

Ikiwa najisi hajayabadilisha maji chochote katika hizo sifa tulizo zitaja hapo, basi maji hayo hayatafaa kuyatumia katika kauli sahihi ya wana wa vyuoni.

Vile vile inafaa kuyatumia maji yaliyobaki kwenye chombo baada ya kunywewa, isipokuwa ikiwa ameyanywa mbwa au nguruwe maji hayo yatakuwa ni najisi hayatafaa kujitwaharisha.